# Kristo 3



Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2021

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.





MATHAYO 3:1-6; MARKO 1:1-6; LUKA 3:1-6; JOHANA 1:6-8






MATHAYO 3:7-10, LUKE 3:7-12




MATHAYO 3:11-12, MARKO 1:7-8, LUKA 3:13-18






MATHAYO 3:13-15, MARKO 1:9, LUKA 3:21




MATHAYO 3:16-17, MARKO 1:10-11, LUKA 3:22-23


ASANTE YOHANA.
HUYU NDIYE!
HUYU NDIYE NILIYEONGEA KUMHUSU!
ALIYE NYUMA YANGU, NILIYESEMA NI MKUU KUNILIKO MAANAKE ALIKUWA KABLA YANGU!
NI NINI KIMEFANYIKA HAPA FILIPO?
SIJUI ANDREA... SIJUI...



YOHANA 1:15




MATHAYO 4:1-2, MARKO 1:12, LUKA 4:1-2






MATHAYO 4:3-4, LUKA 4:3-4





MATHAYO 4:5-7, LUKA 4:9-12



MATHAYO 4:8, LUKA 4:5






MATHAYO 4:9-10, LUKA 4:6-8


KWA HIYO, IBILISI AKAMWACHA,
MPAKA FURSA NYENGINE ILIPOJITOKEZA.
MALAIKA
WAKAJA...
...WALIOMHUDUMIA NA
KUMSHUGHULIKIA HUKO NYIKANI.


NDIO YULE. ANA WAFUASI WENGI.
WATU WANAYASIKIZA MANENO YAKE.
HIYO NI TATIZO KAMA MANENO YAKE NI UONGO AU AMEGEUZA UKWELI.
NJOO TUSKIZE.
MBATIZAJI! KIDOGO!
TUNA MASWALI YA KUKUULIZA!
NDIO, NDIO, KUNA NINI?
SAWA, SASA, TUNA TASHWISHI KIDOGO KUHUSU TULICHOSKIA JUU YA MAFUNDISHO YAKO.
SIFUNZI LOLOTE LISILO KWELI.
WENGINE WASEMA UNADAI KUWA KRISTO. MASIHI.
WEWE NDIYE?
LA, HAPANA!
NIMESEMA MARA KWA MARA BILA HAYA, MIMI SI KRISTO!
WEWE NI NANI BASI? ELIYA?
LA!
WEWE NDIYE NABII?
LA.
WE NI NANI?
TAFADHALI TUELEZE. LAZIMA TUPELEKE JIBU KWA WALIOTUTUMA.


MWATAKA KUJUA MIMI NI NANI?
MIMI NI SAUTI ILIAYO NYIKANI.
SAUTI INAYOSEMA, "INYOSHENI NJIA YA BWANA!"
SAUTI ALIYOIONGELEA NABII ISAYA MIAKA MINGI ILIYOPITA!
WASEMA WEWE SIYE KRISTO! WEWE SIO ELIYA! WEWE SIYE NABII!
BALI WABATIZA!
MBONA UFANYE HIVI?
UBATIZAJI WANGU UNAASHIRIA UTAKASAJI WA MAJI!
LAKINI KUNA MMOJA KATI YENU MSIYEMJUA ATAKAYEKUJA NYUMA YANGU!
MWANA-KONDOO WA MUNGU AICHUKUAYE DHAMBI YA DUNIA!
NAMTAYARISHIA NJIA INGAWA SISTAHILI KUILEGEZA GIDAMU YA KIATU CHAKE!
HAKUSEMA LOLOTE LA KUKUFURU!
NI KWELI, ANASEMA TU YANAVYOSEMA MAANDIKO: MASIHI YWAJA!
AH! MANENO YAKE "YA KWELI" YATOKA KWA KINYWA CHA MWENYE KIBURI MPAKA ASEME NI YEYE ISAYA ALIONGEA JUU YAKE!
NA MAKUHANI NA WALAWI WAKARUDI YERUSALEMU KUTOA RIPOTI.
HUKU JOHANA AKIENDELEA KUONGEA KUHUSU "MWANA-KONDOO WA MUNGU..."


...NA NILIONA ROHO AKISHUKA NA KUTUA JUU YAKE KAMA HUA!
MBELENI NILIMFAHAMU LAKINI SIKUELEWA ALIKUWA NANI!
LAKINI ALIYENITUMA KUBATIZA KWA MAJI ALINIAMBIA HIVI:
"YEYE AMBAYE UTAMUONA ROHO AKISHUKA JUU YAKE, HUYO NDIYE ABATIZAYE NA ROHO MTAKATIFU!"
NAMI NIMEONA NA NASHUHUDIA, NAJUA KUWA NI MWANA WA MUNGU!
YOHANA...
TAZAMA!!!
MWANA-KONDOO WA MUNGU!!!


ENDA!
ENDA!
RABI!!!
MWALIMU!!!
WATAKA NINI? NI NINI UNACHOKITAFUTA?
RABI...
UNAKAA WAPI?
NJOONI NAMI MARAFIKI ZANGU MUONE.
JOHN 1:37-39


NA WAKAENDA.
RABI NTARUDI SASA HIVI...
ANDREYA WAEZA KUWA WAENDA WAPI?
NAENDA KUMLETA KAKANGU... HATAAMINI NILYESHINDA NAYE!
SIMONI!
SIMONI!!!
ANDREYA?
KUNA NINI?
SIMONI, NI YEYE!
KWA KWELI NI YEYE!
YUKO HAPA! NIMESHINDA NAYE!
NANI YUKO HAPA? MBATIZAJI?
LA! YULE AMBAYE MBATIZAJI ANASHINDA AKIZUNGUMZIA JUU YAKE!
MASIHI
MASIHI?
HAPA?


YAPASWA USIKIE MAMBO ANAYOYASEMA!
NILIDHANI YOHANA NI KAMA MANABII MASIHI ANAPOHUSIKA...
KUTUAMBIA KUHUSU JAMBO LILOPASWA KUTENDEKA LAKINI BAADA YA VIZAZI!
HA! HA! LA! NI SASA! NI SASA!!!
JAMBO!
JAMBO RABI. KAKANGU AMENIAMBIA MENGI KUKUHUSU.
WEWE NI SIMONI MWANA WA YOHANA.
LAKINI UTAITWA PETERO...
PETRO? "JIWE," EH? JINA ZURI KWA KAKANGU!!!
NDIO. UTAITWA PETRO.
NA WAKASHINDA NAYE.
HAYA, WAONAJE?
NI MWANAMUME WA AJABU...
SASA NJOO! LAZIMA TWENDE KWENYE VYOMBO!
TWAPOTEZA MDA TAYARI! TAYARI MAJI YASHAKUWA BARIDI NA SAMAKI WANAELEA!


SIKU ILIYOFUATA.
...ASUBUHI NA JIONI, MWANA-KONDOO ATOLEWA KAFARA KWA DHAMBI ZETU, NA ALIYE NYUMA YANGU NI MWANA-KONDOO AMBAYE NABII ISAYA ALIMTAJA...
FILIPO!
MARAFIKI ZAKO WAKO WAPI?
NI WAVUVI. WALIKESHA BAHARINI.
NAENDA GALILAYA.
SAWA... HUKO NDIKO UNAKOTOKA, SIO?
NIFUATE!
BILA SHAKA RABI!
BILA SHAKA!
RABI... KUNA JAMBO MOJA NINGEPENDA KUFANYA KABLA HATUJAENDA...


"...AKAOTA NDOTO, NA TAZAMA, NGAZI IMESIMAMISHWA JUU YA NCHI NA NCHA YAKE YAFIKA MBINGUNI; TENA TAZAMA, MALAIKA WA MUNGU WAPANDA NA KUSHUKA JUU YAKE..."
NGAZI KATI YA MBINGU NA NCHI... KATI YA MUNGU NA MWANADAMU...
NATHANAELI!!!
NATHANAELI LAZIMA UJE NAMI.
TUMEWAONA WALIOANDIKWA NA MUSA KWENYE SHERIA!
YULE ALIYEONGELEWA NA NABII!
MASIHI? UNA UHAKIKA HIVYO NDIVYO UNAVYOSEMA?
NJOO UKUTANE NAYE!
JINA LAKE NI YESU! YESU WA NAZARETI!!!
NAZARETI! KIJIJI KIDOGO NAMNA HIYO!
NA KILE KITUO CHA NJE CHA ROMA KARIBU HIVYO...
NILIYOYASIKIA KUHUSU WATU HUKO...
NENO JEMA LAWEZA KUTOKA NAZARETI?
ONGEA NAYE UONE!
TAZAMA, MWISRAELI KWELI KWELI!
MWANAMUME MKWELI NA WA KWELI!
NA WAJUAJE LOLOTE JUU YANGU?
NILIKUONA!
KABLA FILIPO AKUITE NILIKUONA UKIKAA CHINI YA MKUYU!
MAHALI PEMA PA MAOMBI NA KUTAFAKARI NA KUJIFUNZA SHERIA...


RABI, WEWE NI MWANA WA MUNGU, SIVYO?
U MFALME WA WAFALME.
KWA HIYO WAAMINI MAANAKE NILIKWAMBIA NILIKUONA CHINI YA MKUYU?
NATHANAELI NA BARTHOLOMAYO, HAMJAONA LOLOTE BADO!
NAWAAMBIENI MTAONA MBINGU ZIKIFUNGUKA!
MALAIKA WA MUNGU WAKIKWEA NA KUSHUKA JUU YA MWANA WA ADAMU!
NGAZI KATI YA MBINGU NA NCHI...KATI YA MUNGU NA BINAADAM...
YESU NA WAFUASI WAKE WAKAENDA NYUMBANI KWAO YESU HUKO GALILAYA NA WALIPOKUWA HUKO WALIALIKWA KWENYE SHEREHE YA ARUSI KWA KIJIJI CHA KARIBU CHA KANA.


SIWEZI KUSEMA HAYA NDIYO NILIYOYATARAJIA MASIHI ALIPOSEMA NIMFUATE!
NINASHUKU HATAFANYA VITU VINGI TUNAVYOTARAJIA!
YESU! IPO SHIDA!
WAMEISHIWA NA DIVAI!
MAMA MBONA UNIHUSISHE?
WAKATI WANGU BADO.
WEWE HAPO!
FANYA ATACHOKWAMBIA!
NI MWEREVU, ATASAIDIA KUTATUA SHIDA HII!
JAZENI MABALASI HAYA NA MAJI!
MABALASI HAYA? TWANAWA MIKONO YETU NAYO!
MAJI. TWASHKURU TUNA JAMAA HUYU WA KUTUSAIDIA KUTATUA SHIDA HII.
MARIA ALISEMA TUFANYE ASEMALO! FANYA!
JAZA KOMBE LANGU!
LAKINI BWANA...
UPESI! JAZA KOMBE LANGU!
NAAM BWANA.


MMMM
MMMMM
BWANA HARUSI YUKO WAPI!?!
KAWAIDA WATU HUANDAA DIVAI ILIYO NJEMA KWANZA NA KULETA ILIYO DHAIFU WAKATI HISIA ZETU NI DHAIFU!
LAKINI YULE MJANJA AMENGOJA MPAKA SASA KUANDAA DIVAI ILIYO BORA, NA NI BORA ZAIDI KULIKO DIVAI YOYOTE ILE NIMEWAHI KUONJA!
LAKINI... MABALASI YALE...
NAJUA! MAJI! NILIONA!
IANGALIE!
INUSE!
IONJE!
NI BORA ZAIDI NILIYOWAHI KUONJA!
HII ILIKUWA MWANZO WA ISHARA ZA MIUJIZA YA YESU
NA UFUNUO HUU WA UTUKUFU WAKE WAFUASI WAKE WALIWEKA IMANI YAO NDANI YAKE.



# HADITHI YA ASKARI

## "INYOOSHENI NJIA"




MBONA HUKUSEMA HIVI HAPO MWANZONI?
INGETUEPUSHA TAABU NYINGI SANA!
HAKIKISHA KUNA YA KUTUTOSHA MIMI NA MWENZANGU YEHOYAKIMU HAPA, NA WENZETU WENGINE...
...EH, EZRA...YUPO NDANI AU...
KWELI, HAKIKA, "EZRA..."
WEWE KUNIULIZA MASWALI?
LA HASHA!
TOSHA!
"EZRA?"
UNA TATIZO NA EZRA?
KWA SABABU KAMA UNAYO NAWEZA KUCHUKUA GAWO LAKE BADALA YA KUGAWA NAWE!
HAPANA, HAPANA... NITACHUKUA KIPANDE CHAKE.
LAKINI "EZRA"?
NILIJITAHIDI VILIVYO!
ASKARI!!!
BWANA! TULIKUWA . . . AH, HATUKU . . .
NYAMAZA! NIMEONA ULICHOFANYA NA UNGEFANYA YOTE KWA UPOLE ZAIDI!
LAKINI SIKO HAPA KWA HAYO!
TWAWEZA KUKUHUDUMIA VIPI BWANA?
WEWE TU YEHOYAKIMU!
NAHITAJI MTU NINAYEWEZA KUMUAMINI.
MIMI JE? NITALINDA MLANGO PEKE YAKE?
"EZRA" AWEZA KUKUSAIDIA, ASKARI!


USHASKIA KUHUSU MBATIZAJI?
ABATIZA WATU NDANI YA YORDANI, SIO?
AOSHA DHAMBI ZAO AU KITU KAMA HICHO.
NDIYE YULE
WALIMVUMILIA MAANAKE ALIKUWA ANAHIMIZA WATU WAWE RAIA WAZURI.
KUNYWA! KULA! NI YAKO YEHOYAKIMU!
LAKINI BILA SHAKA UMESIKIA KUWA HERODE ANTIPASI KAMCHUKUWA MKEWE KAKA YAKE FILIPO . . .
NDIO, NIMESIKIA.
MWANAMUME HUYU YOHANA -- NDILO JINA LA MBATIZAJI -- AMEKASHIFU MATENDO YA MFALME WETU.
ASEMA HERODE AHITAJI KUTUBU DHAMBI, KUWA HAYUKO JUU YA SHERIA ZA MUNGU.
HAJASHAWISHI MTU YEYOTE KWA UASI AU KITU CHA NAMNA HIYO--
BADO.
HAKIKA.
ENDA KAMWANGALIE MBATIZAJI.
PATA MUELEKEO CHA ANACHOSEMA NA VILE AMBAVYO WATU WANAKICHUKULIA KISHA UPIGE RIPOTI KWANGU.
SAWA KABISA BWANA --
"-NITAJITAHIDI."



NIAMBIE WAJUA NINI KUHUSU MBATIZAJI HUYU?
MUNGU AONGEA KUPITIA KWAKE!
MATAMSHI YAKE YANA NGUVU!
NIMEKUJA KUONA VITUKO HIVI MWENYEWE!
FAMILIA NZIMA YA KAKA YANGU ILIBATIZWA JUMA LILILOPITA!
ATULETEA UKWELI WA NENO LA MUNGU.
ASEMA ANYOOSHA NJIA YA MASIHI!
MASIHI? KWELI?
LAKINI MATAYARISHO YA YOHANA NI MATAYARISHO YA MOYO! SIO YA UPANGA!
NA HERODE JE?
YEYE JE? DHAMBI ZAKE ZIMETENGWA KUTOKA KWA SHERIA YA MUNGU?
MFALME DAUDI ALIPOTENDA DHAMBI MUNGU ALIKUBALI DHAMBI YAKE KWA KUWA N MFALME?


WEWE, RAFIKI, HUFAI KUWA NA WASIWASI SANA KUHUSU DHAMBI ZA MFALME WETU!
UNAFAA UWE NA WASIWASI KUHUSU DHAMBI ZOTE ZINAZOENDELEA HUMO . . .
HAYO NDIO UJUMBE WA YOHANA UNAGUSIA, NA ANGECHOMWAMBIA WEWE AU HERODE . . . AU MIMI . . . AU WEWE!
MATAMSHI YAKE NI HATARI.
YANAKARIBIA KUWA UZUSHI!
LAKINI TWAWEZA VIPI KUMLAANI MTU ANAYEWAITA WATU KWA USAFI?
MDA MFUPI ULIOPITA NILIONA KITU CHA AJABU MNO!
KUNA MTU--WENGINE WASEMA NI BINAMUYE YOHANA--ALIKUJA AKIULIZA KUBATIZWA!
HUA HUYU ALIPEPEA CHINI TOKA MBINGUNI NA SAUTI IKASEMA HUYO JAMAA NI MWANA WA MUNGU!
GHAFLA UJUMBE WA YOHANA WABADILIKA TOKA "MASIHI YWAJA, KUWENI TAYARI" MPAKA "MASIHI AMEKUJA!"
YOHANA AZUNGUMZIA MASSIAH, KAMA TULIVYOTAKA MIAKA YOTE HII: MTU WA KUVUNJA NIRA YA FALME ZOTE HIZI ZILIZOTUONGOZA KWA MIAKA MINGI.
SIWEZI KUHUZUNIKA KAMA HERODE ANTIPASI NA WARUMI WANAOTAWALA WANGEANGUSHWA...
LAKINI NAFIKIRIA KUNA JAMBO LENGINE LINAENDELEA HAPA, JAMBO TUSILOLITERAJIA. JAMBO TUSILOJUA TUNALITAKA!
AU KULIHITAJI.


TUBUNI DHAMBI ZENU!
KAMA NLIVYOSEMA MIMI NDIYE MTANGAZAJI NAMUANDALIA NJIA ALIYE MKUU KUNILIKO!
TAZAMA AMEKUJA! NIMEMUONA! KAMA WALIVYOFANYA WENGI WENU!
BWANA! MIE NI ASKARI!
NIFANYE NINI KUJITAYARISHA KWA MASIHI HUYU UNAYEMTAJA?
NITAKUBATIZA NA MAJI NA UTAKAPOONDOKA MAHALI HAPA UTAKUMBUKA KUWA MAHALI HAPA NDIPO ULIONDOA MOYO WAKO KWA UOVU NA KUUGEUKIA UTUKUFU WA BWANA!
LAKINI UENDAPO NYUMBANI FANYA AMBAVYO NABII ATAKUSIHI!
WAPE MASKINI! WALINDE WAJANE NA MAYATIMA!
ASKARI, EH?
WAJUA NTAKACHOKISEMA TAYARI, SIO?
USIIBE PESA!
TOSHEKA NA MALIPO YAKO!
USISINGIZIE WATU...
TAYARISHA MOYO WAKO!
"ALIKUWA SAWA. NILILIULIZA SWALI --"


-- LAKINI ALIPOKUWA ANAONGEA NILIJUA TAYARI ALICHOKIPANGA KUSEMA.
NAJUA . . . NI VILE . . .
BILA SHAKA! WAJUA INACHOMAANISHA KUWA ASKARI ANAYEMTUMIKIA HERODE KAMA VILE HUYU YOHANA!
KWA HIYO ULIBATIZWA!
LA . . .
HUYU MBATIZAJI SIO TISHIO LAKINI.
SIO KAMA WALE MANABII WENGINEO WANAOTOKEZEA MARA KWA MARA. HAITANII AINA YOYOTE YA UASI.
ANAWAITA WATU WETU, WATU WA MUNGU, WAWE WAZURI. WAWE . . . WACHA MUNGU.
NA ALIONGEA KUHUSU "MASIHI"? "KRISTO"?
KUNA UVUMI . . .
ALISEMA BWANA.
YASEMEKANA AMEMUONA ATAKAYEKUWA MASSIAH WETU.
LAKINI UJUMBE WA YOHANA NI WA KIROHO, SIO WA KISIASA.
KUNA UVUMI MWENGINE. MFALME NA MKEWE HAWAFURAHIKII ANAVYOSEMA YOHANA.
KAMA NINGALIKUWA WEWE SINGEENDA KUJIUNGA NA DHEHEBU LAKE WALA CHOCHOTE!
ASANTE YEHOYAKIMU.
HIKI NI KIDOGO ZAIDI KWA KUSHUGHULIKA KWA HISANI YA WALIPA USHURU WETU WAAMINIFU...
ILA KAMA WAFIKIRIA MBATIZAJI HANGEFURAHIKIA.
BILA SHAKA WAWEZA KUIPEANA KWA MASIKINI!


ENHE, KIJIKAZI CHENU KILIENDAJE JANA?
ILIKUWA . . . YA AJABU.
NILISIKIA ULIPATA KWENDA MTONI AU KITU KAMA HICHO.
JAMANI SIO HAWA WAWILI TENA ...
MTUMISHI AMENIOMBA NIRUDI LEO KUZUNGUMZA JUU YA USAFIRISHAJI WA NAFAKA HALISI KUTOKA MISRI.
ITANIGHARIMU NINI?
RAFIKI YANGU EZRA . . . NA BINAMUYE --
HAMNA BWANA.
TAFADHALI KAA KANDO. MTUMISHI AKUTARAJIA!
N-N-NINI?
NA UONDOKAPO TAFADHALI NITAFUTE. NAHITAJI KUKUREJESHEA KITU ULICHOKIPOTEZA JANA HAPA. MASHILINGI...
UMETUGHARIMU NYONGEZA NYENGINE NZURI!
WAONA WAFANYA NINI YEHOYAKIMU?
KAZI YANGU...
MTUMIKIE MFALME.
NINA HAKIKA HERODE ATAJIGAMBA!
SIZUNGUMZII JUU YA HERODE YARUNI.
MWISHO.

"THE BIBLE EXPLAINED IN EVERY LANGUAGE."





**SUPERBIBLE.TV**